# WILAYA YA NAIROBI

## DARASA LA NNE MUHULA WA TATU

PENPLUS NAIROBI

# KISWAHILI

*MUDA: Saa 1 Dakika 40*

***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa kwa kujaza nafasi moja hadi kumi na tano.***

Fisi ni mnyama ___1___. Yeye na Sungura ___2___ marafiki.

Kila siku wakati ___3___ chakula Fisi alikuwa ___4___ kwa Sungura. Sungura alikuwa anasikia vibaya sana. Chakula ___5___ hakiwatoshi yeye na watoto ___6___. Watoto ___7___ Sungura walikuwa hawashibi. Sungura alitafuta njia ya kumzuia Fisi asiende tena kula chakula. Alifikiri kwa muda, mwisho akapata jibu. Alichukua jiwe ___8___ chuma akalitia motoni mpaka likawa ___9___. Alilipaka mafuta ya ng'ombe. Mara Fisi akaingia. Sungura akamkaribisha vizuri. Akampa ___10___ jiwe lililoonekana kama nyama ___11___ mafuta. Fisi akaanza ___12___ kwa haraka.

Jiwe likakwama ___13___. Fisi ___14___ na kufa papo ___15___.

1. A. mnyenyekevu B. mlafi C. Mvivu D. mkaidi
2. A. walikua B. alikua C. alikuwa D. walikuwa
3. A. wa B. la C. cha D. ni
4. A. akienda B. wakienda C. simama D. akieda
5. A. ilikuwa B. mlikuwa C. kilikuwa D. kilikua
6. A. yake B. wake C. zake D. wao
7. A. cha B. pa C. za D. wa
8. A. la B. wa C. za D. pa
9. A. wekundu B. lekundu C. jekundu D. njekundu
10. A. pale B. zile C. yule D. lile
11. A. kwa B. ya C. katika D. kwenye
12. A. kumeza B. kilimeza C. kurimeza D. meza
13. A. kooni B. mdomoni C. puani D. tumboni
14. A. akaketi B. akasimama C. akaanguka D. akainuka
15. A. mule B. pale C. huko D. hapo

***Kutoka swali la 16 - 30 jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Kamilisha methali: Fuata nyuki ule ______
    A. nta B. asali C. chakula D. jana

***Chagua jibu sahihi kukamilisha sentensi zifuatazo.***

17. Musa ana uvimbe kwenye shingo ______
    A. yake B. lake C. wake D. chake
18. Magari haya ni ______
    A. mibovu B. mabovu C. bovu D. mbovu

***Geuza sentensi kwa wingi***


19. Wewe utamsaidia mgonjwa huyu.
    A. Wewe utawasaidia mgonjwa huyu
    B. Nyinyi utawasaidia wagonjwa hawa
    C. Nyinyi mtawasaidia wagonjwa hawa.
    D. Wao watawasaidia wagonjwa hawa.
20. Yule mtu mrefu ni mjomba wako.
    A. Yule mtu warefu ni wajomba wako.
    B. Hawa watu warefu ni mjomba wao.
    C. Yule watu mrefu ni wanjomba wako.
    D. Wale watu warefu ni wajomba wako.

***Chagua neno sahihi ulitumie kuzikamilisha sentensi zifuatazo.***

21. Mtoto wa kaka au dada ni ______
    A. ndugu B. mjukuu C. ami D. mpwa
22. Jiko la makaa huitwa ______
    A. Seredani B. Mafiga C. Stovu D. Kichemuo

***Chagua jibu sahihi cha kitendawili kifuatacho.***

23. Halo! Halo mpaka Njabini.
    A. Saa B. Rununu C. Redio D. Runinga
24. Umbo hili huitwa?



    A. Mche duara B. Mche mraba C. Mche mstatili D. Pia

***Kamilisha sentensi.***

25. Walimu ______ wanafunza kiswahili?
    A. yupi B. ngapi C. ipi D. wapi

26. Jua hutua upande gani kila siku?
A. Mashariki B. Magharibi
C. Kaskazini D. Kusini

27. Ugonjwa wa kuanguka na kuzimia ni upi?
A. Kifafa B. Kichocho
C. Kifaduro D. Kichaa

***Andika kwa tarakimu***

28. Kondoo elfu saba mia nane themanini na wanane ____
A. 7868 B. 7487 C. 7888 D. 7880

29. Jina kitabu liko ngeli gani?
A. KI-VI B. LI-YA
C. I-ZI D. A-WA

***Kanusha sentensi hii.***

30. Ninaandika barua
A. sitaandika barua B. sijaandika barua
C. sitaiandika barua D. siandiki barua

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.***

Musa alikuwa mvulana aliyezaliwa katika familia tajiri. Wazazi wake walijaliwa utajiri usio kifani. Maisha kwao nyumbani yalikuwa ni raha mstarehe. Alipofikisha umri wa kuenda shuleni, wazazi wake walimpeleka shule moja ya kifahari iliyoitwa shule ya msingi ya Suwerwa. Musa alisoma vizuri sana na walipofanya mtihani aliibuka nambari moja mwishoni mwa muhula. Musa alikuwa mwanafunzi mwenye nidhamu na heshima kwa walimu, wazazi na watu wote. Aliendelea kuongoza darasani kila walipofanya mtihani.

Alipojiunga na darasa la nne maisha ya Musa yalianza kubadilika kwa sababu aliungana na rafiki wabaya tabia yake ikabadilika akaanza kuwa mtoto mtundu asiye na nidhamu. Wazazi wake walimwonya Musa lakini hakusikia aliendelea kuwa mtundu. Katika masomo yake Musa alianza kurudi nyuma akawa anaburura mkia kila walipofanya mtihani. Baadaye Musa alikataa shule na kuungana na rafiki wabaya waliowaibia watu mjini. Siku moja Musa alipigwa risasi na kuaga dunia papo hapo.

31. Musa alikuwa ____
A. mzee B. mvulana
C. msichana D. kaka

32. Familia ya Musa ilikuwa ____
A. maskini B. tajiri C. kubwa D. ndogo

33. Musa alipelekwa shule ya ____
A. kifahari B. mtaani
C. mjini D. kijijini

34. Kinyume cha tajiri ni ____
A. maskini B. mkwasi
C. mtundu D. raha

35. Musa aliungana na rafiki ____
A. wema B. wabaya C. warefu D. wazuri

36. Jina la shule aliyosomea Musa ni ____
A. Suswa B. Satuma C. Sawerwa D. Mjini

37. Musa na rafiki zake waliwaibia watu ____
A. njiani B. shuleni C. darasani D. mjini

38. Kuburura mkia ina maana ya;
A. kuwa wa kwanza B. kuwa wa pili
C. kuvuta mkia D. kuwa wa mwisho

39. Musa aliuliwa na ____
A. raia B. watu C. polisi D. wazee

40. Ni nini maana ya kuaga dunia.
A. kulala B. kufa C. kuanguka D. kuzirai

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.***

Miti ina faida nyingi sana kwetu binadamu na wanyama wengine. Kwanza miti hutupa mbao za kujenga nyumba zetu. Miti pia hutupa matunda ambayo huwa matamu kama asali. Miti vilevile hutukinga kutokana na jua kali kwani inatupa kivuli.

Miti vilevile hutupa kuni tunazotumia kupikia chakula chetu. Hizi kuni vilevile hutupa joto nyumbani mwetu. Miti mingi kwa pamoja huitwa misitu. Misitu ni makao ya wanyama wengi kama vile, simba, chui, kifaru na fisi. Mti husaidia kupafanya mahali pawe parembo na pa kupendeza.

Miti husaidia kuvuta mvua na kuzuia mchanga kubebwa na maji na upepo. Serikali yetu inatuhimiza tupande miti mingi na tusiikate ovyo ovyo kwani miti ni muhimu sana katika maisha yetu.

41. Miti ina faida kwa ____
A. binadamu B. wanyama
C. binadamu na wanyama D. nchi

42. Nini hatupati kutoka kwa miti?
A. mbao B. maji
C. matunda D. kivuli

43. Matunda tunayopata kutoka kwa miti ni matamu kama ____
A. asali B. sukari
C. peremende D. pipi

44. Asali hutengenezwa na mdudu yupi?
A. mende B. panzi C. mbu D. nyuki

45. Miti mingi ikikua pamoja huitwa:-
A. mipera B. miembe C. misitu D. milima

46. Wanyama wangapi wametajwa ambao huishi misituni ____
A. watatu B. wanne C. sita D. watano

47. Kukiwa na jua kali miti hutupa ____
A. mwangaza B. mvua C. kivuli D. mwavuli

48. Mchanga hubebwa na ____
A. kivuli B. mvua
C. lori D. maji na upepo

49. Mnyama aliyetajwa ambaye ni mlafi sana ni:-
A. ndovu B. chui C. fisi D. kifaru

50. ____ inatuhimiza tupande miti mingi.
A. Sheria B. Serikari C. Siri D. Shule